**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANDENI**

**MTIHANI WA ROBO MHULA KIDATO CHA PILI 2023**

**MSIMBO: 015** **SOMO: ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

**MUDA : MASAA 2:30**

**SEHEMU A (Alama 15)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Katika vipengele (i) - (x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi yake katika kisanduku ulichopewa upande wa kulia.

(i) "…. Je wanaweza kuwa sawa wale wanaojua na wale wasiojua?" [39:9]. Ni vipi wanatofautiana watu wa aina mbili waliotajwa katika aya hii?
A. Kwa kusoma hatua nyingi za kielimu B. Kwa wingi wa tafiti za kielimu zilizofanywa
C. Kwa ufanisi katika utendaji wao D. Kwa kuwa na uwezo mkubwa wa ufanisi.

(ii) Bwana Kippo haonekani kushirikiana na wenzake katika shughuli za maendeleo akiamini kuwa kwa kufanya hivyo atakuwa karibu na Mola wake. Je, Bwana Kippo ni muumini wa dini gani?

A. Utawa B. Ukafiri C. Uislamu D. Ushirikina.

(iii) Katika jamii hushuhudiwa watu wanaoingia katika Uislamu wakitamka shahada zote mbili; hawawezi kumshuhudia Allah (s.w) mpaka amshuhudie na Muhammad (s.a.w). Unafikiri ni kwanini inakuwa hivyo?
A. Kwa sababu Mtume (s.a.w) ni wa kwanza kuumbwa B. Kwa sababu Mtume (s.a.w) ndiye Mtume wa mwisho
C. Kwa sababu Mtume (s.a.w) ndiye aliyefundisha kumjua Allah mmoja
D. Kwa sababu Mtume (s.a.w) pekee ndiye aliyepewa swala tano.

(iv) "Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu". [51:56] Ni upi uhusiano uliopo kati ya nguzo tano za Uislamu na lengo la kuumbwa lililotajwa katika aya hiyo?
A. Muislamu akitekeleza nguzo tano ipasavyo atafikia lengo la kuumbwa kwake
B. Nguzo tano za Uislamu ni nyenzo ya kumuwezesha Muislamu kufikia lengo la kuumbwa
C. Nguzo tano za Uislamu humtofautisha Muislamu na asiyekuwa Muislamu
D. Nguzo tano za Uislamu ndio lengo kuu aliloumbiwa Muislamu.

(v) "Enyi mlioamini mmelazimishwa kufunga (swaumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla

yenu". [2:183]. Makusudio hasa ya faradhi iliyotajwa katika aya hii ni yapi?
A. Kuwezesha watu wote kuonja ladha ya njaa B. Kuwezesha kufutiwa dhambi zetu zote
C. Kuadhimisha tukio la kushuka Qur'an D. Kujifunza kuchunga mipaka ya Allah (s.w).

(vi) Daktari Ashur anapenda kusoma Qur'an kila siku baada ya swala ya alfajir. Ni ipi si adabu inayopaswa kuzingatiwa na Daktari Ashur katika usomaji wake?
A. Kuanza kwa kumlaani shaitwani B. Kuanza kwa kusoma Bismillah
C. Kusoma akiwa amevaa kanzu na kofia D. Kusoma akiwa msafi na twahara.

(vii) Qur'an ilipokuwa inashushwa ilipitia vituo maalumu katika mchakato wake. Ni kundi lipi la maneno linaeleza vyema vituo hivyo muhimu kwa mpangilio?
A. Lawhi Mmahufudh – uwingu wa dunia – Jabal Hira
B. Jabal Hira – Lawhi Mmahfudh – uwingu wa Dunia
C. Uwingu wa Dunia – Lawhi Mmahfudh – Jabal Hira
D. Lawhi Mmahfudh – Laitul Qadri – Jabal Hira.

(viii) Amina alipatwa na hasira baada ya kusikia jirani zake wakimtukana Mtume (s.a.w). Kwa mafundisho ya Mtume (s.a.w) unamshauri Amina afanye nini ili ajizuie na hali hiyo?

A. Amlaani shaitwani kwa kusema "Au'udhubillah mina shaitwan rajim"
B. Amlaani shaitwani kwa kusema Allah. Akbar Laailaaha illa Anta"
C. Alipize kisasi kwa jirani zake kwani kisasi ni haki
D. Asiwapige bali aende kwa Kadhi au hakimu akashitakiwa

(ix) Makosa yaliyokuwa yanafanyika kipindi cha Jahiliyyah bara Arab, baadhi yake hata zama hizi yanafanyika tena wazi wazi. Ni upi mfano wa makosa hayo?
A. Kuzika mabinti wakiwa hai
B. Kutokuwa na serikali inayotambulika
C. Wanawake waliofiwa na waume zao kurithiwa kwa nguvu
D. Wanawake kucheza ngoma/muziki uchi hadharan.

(x). Bibi Zainab anamiliki Shamba lenye machungwa, zabibu, mpunga, maembe na mahindi. Bainisha mazao ambayo anapaswa kuyatolea Zaka ikiwa yamefkia Nisab.

A. Zabibu , Mpunga na Maembe B. Zabibu, Maembe na Mahindi

C. Mahindi, Mpunga na Zabibu D. Mahindi, Maembe na Zabibu.

2. Oanisha Fungu za Sunna zilizopo katika Orodha A na majina ya Funga hizo katika Orodha B kisha andika herufi ya jibu sahihi Kwa kila kipengele katika kijitabu chako Cha kujibia .

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| (I) Kufunga tarehe 12,13,na 14 katika miezi ya Hijriya<br><br>(ii) Kunga tarehe 9 katika mwezi wa Dhul Hijja | A . Funga ya Ashura<br><br>B. Funga ya kafara<br><br>C. Funga siku nyeupe |

| | |
|---|---|
| (iii) Kufunga tarehe 10 katika mwezi wa muharram | D. Sunna Nabii Dawud |
| (iv) Funga muakkada kila mwezi wa 10 Hijriya | E. Sitta Shawwal |
| (v) Kufunga kila baada ya siku Moja | F. Funga ya Arafa |
| | G. Masiku meusi |

**SEHEMU B ( Alama 70)**

Jibu maswali yote.

3. Wanakijiji wa Vumi wana fikra zisizokuwa sahihi kuhusu Mwenyezi Mungu lakini wanashauku ya kutaka kumjua. Ni njia gani Tano zinaweza kuwasaidia kutimiza azma yao?

4. (a) Elezea tofauti ya stara ya vazi la mwanaume na stara ya vazi la mwanamke

(b) Bainisha Sifa Tano za vazi la kijana wa kiislamu

5. Fafanua lengo la kila nguzo kati ya nguzo tano za Uislamu.

6. (a) Bainisha masharti matatu ya maiti anayestahiki kuswaliwa.

(b) Ainisha Sunna Tano (5) za Swala ya maiti

7. Bainisha Kwa ufupi Mafunzo matano ya Suratul Lahab Kwa jamii ya waislam.

8. (a) Toa Maana ya Fiqh

(b) Ainisha misingi mitatu ya Fiqh

(c) Eleza tofauti ya Fiqh ibadat na Fiqh muamalat.

9. (a) . Bainisha Kwa kifupi Sifa Tatu za muumini wa kweli

(b) . Eleza nguzo Tano za matamshi katika Swala

**SEHEMU C (Alama 15)**

10. Wanafunzi wa shule ya sekondar Ubungo Islam walisafiri safari ya kimasomo kutoka Dar es Salaam kuja shuleni kwenu . Ukiwa umebobea katika taaluma ya ibada ya Funga wafafanulie faida Tano (5) za kutekeleza Funga ya mwezi mtukufu wa Ramadhan .